



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



Kumb. Na. LMC/J.20/3/VOL.III/66

09/10/2023

**TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA
NAFASI I**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi anawatangazia Wananchi wenye sifa ili kutuma maombi ya kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Manispaa ya Lindi.

Tangazo hili limetolewa baada ya Mwenyekiti aliyekuwepo kumaliza muda wake.

SIFA ZA MUOMBAJI

- i. Awe ni mkazi wa eneo la Manispaa ya Lindi
- ii. Awe na Umri wa miaka 55 – 70 na isiyozidi 70
- iii. Asiwe Mwajiriwa wa Umma (Awe amestaafu kazi)
- iv. Awe na taaluma na uzoefu katika fani ya Sheria, Utawala au Usimamizi wa Rasilimali Watu
- v. Awe na akili timamu na asiye na rekodi ya makosa ya Jinai (Rushwa, Wizi, n.k.
- vi. Aliemaliza muda wake anaruhusiwa

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:

- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za Vyeti vya Elimu na mafunzo ya taaluma husika na yapitishwe kwa Mwenyekiti wa Mtaa anaishi mwombaji


- > Maombi yaambatishwe pia na picha 2 za passport za rangi za sasa za mwombaji pamoja na namba za simu ya mkononi.
- > Mwombaji aambatishe Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

ANUANI

Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Halmashauri ,
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P 1070,
LINDI.

Muda wa kuwasilisha maombi ni kuanzia tarehe 9/10/2023 hadi 23/10/2023 saa 9:30 Alasiri.



Juma A. Mnwele

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHURI YA MANISPAA
LINDI.**



